

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA MARA:
Simu Na.028 2621055
Nukushi .Na.0282621264
Barua pepe: ded@bundadc.go.tz
Tovuti www.bundadc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 126,
BUNDA.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. HB/W:20/33/343

25/05/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda anawatangazia Watanzania wote wenye sifa nafasi za kazi za **Katibu Mahsusi Daraja la III**. Nafasi hizi za ajira zinatokana na Kibali cha ajira kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia barua yake yenye Kumb. Na. FA.97/228/01/9 ya tarehe 13 Mei, 2022.

1.0 KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III - NAFASI NNE (04).

1:1 MAJUKUMU YA KAZI

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miada, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI.

- Awe na elimu ya Kidato cha Nne au Sita.
- Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua Tatu.
- Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotarbuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

1.3 MSAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali kwa kuanzia na TGS B1.

2.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa na Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA.
- Waombaji waambatishe maelezo binafsi (Detail CV) yenye anuani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- Maombi yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma yaani nakala ya vyeti vya Kidato cha Nne au Sita pamoja na vyeti vya taaluma (Professional Certificate from respective board, computer certificate) na picha mbili za rangi za hivi karibuni.
- Testimonials, Provisional of Results, Statement of Results, Hati ya matokeo ya Kidato cha Nne (Form IV) na Kidato cha Sita (Form VI) havitakubalika kabisa.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (NECTA na NACTE) na taarifa ya ulinganifu iambatanishwe kwenye maombi.
- Waombaji wa nafasi za ajira waliostaafishwa, waliofukuzwa kazi na kuachishwa kazi katika utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza tofauti na hapo maombi hayo hayatapokelewa.
- Kichwa cha barua kitaje nafasi ya Kada unayoomba kwa ufasaha.
- Barua ya maombi isainiwe na mwombaji mwenyewe tofauti na hivyo maombi hayo yatakataliwa.
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usahili kupitia namba za simu na anuani watakazotumia kwenye barua ya maombi ya kazi.
- Barua zitakazoletwa kwa mkono hazitapokelewa.
- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 08 Juni, 2022 saa 9:30 Alasiri.
- Maombi yote yatamwe kwa njia ya Posta kupitia anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 126,
BUNDA.

Tangazo ili limetolewa na:-



Changwa M. Mkwazu
Mkurugenzi Mtendaji (W)

**BUNDA DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
BUNDA DISTRICT COUNCIL**

NB:- Tangazo ili linapatikana kwenye mbao zote za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, nje ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda na kwenye tovuti (website) ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambayo ni www.bundadc.go.tz.